

# UKWELI UNAPASHWA KUJUWALI.

SASA  
INATOLEWA KWA  
WENYE UMRI  
WA MIAKA 5 NA  
KUENDELEA

MLINDE MTOTO WAKO.



LINDA JAMII YAKO.

## Watoto na vijana watakuwa salama zaidi wanapokamilisha dozi za chanjo ya COVID-19.

Chanjo hiyo inalinda kila mtu, wakiwemo watoto na vijana, dhidi ya kuambukizwa COVID-19. Chanjo hiyo pia inazuia watoto na vijana kutokana na kuugua vibaya sana ikiwa wataugua.

Kuna aina mpya za COVID-19 ambazo huenea kwa urahisi zaidi na zinaweza kusababisha dalili kali zaidi. Chanjo hukulinda dhidi ya aina tofauti za virusi hivi.

## Kuchanja watoto na vijana hulinda jamii nzima.

Watu ambao wamepata chanjo zote za COVID-19 wana uwezekano mdogo wa kueneza virusi kwa wengine. Mtoto aliyefikisha umri unaohitajika anapopewa chanjo inalinda:

- Familia na marafiki zao ambao bado hawajapata chanjo.
- Wakongwe na watu wenye matatizo ya kiafya ambao wako katika hatari kubwa ya kuugua sana wanapoambukizwa COVID-19.

Kadri watoto na watu wazima wanavyoendelea kupata chanjo, itakuwa rahisi pia kuendeleza masomo shuleni na shughuli za kibiashara.



## SALAMA NA MADHUBUTI

- Hakuna chanjo nyingine ambayo usalama wake umechunguzwa zaidi ya chanjo hii nchini Marekani.
- Chanjo hii imethibitishwa kuwa salama kwa watoto, vijana na watu wazima, ikiwemo kwa watu wa jamii, kabila na umri mbalimbali.
- Chanjo za COVID-19 haziathiri kubalehe au uzalishaji wa siku zijazo. Chanjo hazitafanya mtoto akose kupata watoto wake hapo baadaye.

## INATOLEWA BILA MALIPO KWA WATU WOTE

- Wewe na mtoto wako mnaweza kupokea chanjo ya bila malipo pasipo kujali **hali ya uhamiaji**.
- Wewe na mtoto wako hamuhitaji **kuonyesha kitambulisho** au kuwa na **bima ya afya** kupokea chanjo ya bila malipo.



**NRC-RIM**  
National Resource Center for  
Refugees, Immigrants, and Migrants

# Cha kutarajia

Mtoto wako anapokuwa amepewa chanjo zake za COVID-19, atakuwa salama zaidi anapohudhuria shule, kucheza michezo na anapotembelea marafiki na familia. Kuchanjwa kikamilifu kunamaanisha kupata dozi zote mbili za chanjo, kisha kupata dozi yoyote ya kuimarisha kinga ya mwili anayostahiki.



## Unapokwenda kupokea chanjo:

- Kabla ya muuguzi au daktari kumpa mtoto wako chanjo, atakueleza kuihusu, ataangalia historia ya matibabu ya mtoto wako na ikiwa una swali atakupea fursa ya kuuliza.
- Mtoto wako atahitajika kusubiri kwa dakika 15-30 ili kuhakikisha kuwa hana mzio wa chanjo.



## Athari ni kawaida

Athari HAZIMAANISHI kuwa mtoto wako ana COVID-19.

Athari zinamaanisha chanjo inafundisha mwili wa mtoto wako jinsi ya kupambana na COVID-19.

Athari zisizo kali zinaweza kujumuisha:

- Maumivu au uvimbe kwenye mkono sehemu inayodungwa sindano
- Uchovu
- Maumivu ya kichwa
- Maumivu ya misuli
- Kuhisi baridi
- Joto jingi
- Kuhisi kutapika



## Athari kali ni nadra sana

**Chanjo ni salama. Kuna uwezekano mkubwa kwamba mtoto wako atakuwa na matatizo makubwa kutokana na COVID-19 kuliko chanjo.**

Idadi ndogo ya vijana wamepata athari kama vile moyo kuvimba (inayojulikana kama 'myocarditis' au 'pericarditis') au damu kuganda.

- Athari kali ni **nadra sana**
- Athari kali **zinatibika** na watu wengi walio nazo hupata nafuu
- Chanjo ina faida zaidi kuliko madhara

## WASILIANA NA DAKTARI WAKO ILI UPATE MAELEZO ZAIDI

Zungumza na daktari au muuguzi wa mtoto wako ili upate maelezo zaidi kuhusu chanjo za COVID-19 na chanjo zingine ambazo huenda mtoto wako anahitaji.

